# JARIBIO LA MTIHANI

D003

## DARASA LA SABA

[7]

## MWAKA 2022

Muda: Dak. 40

| JINA LAKO | |
|---|---|
| SHULE YAKO | |

**Malizia Insha yako kwa maneno yafuatayo na uifanye ya kuvutia zaidi.**

.............................................................................. Nilishangaa nisiweze kuamini kuwa nilikuwa nimeepuka hatari hiyo. Moyoni nilimshukuru Mungu kwa kuniokoa.

# JARIBIO LA MTIHANI

D003 **DARASA LA SABA - MWAKA 2022** **[7]**

# KISWAHILI : LUGHA

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kwa yale uliyopewa.**

Kampeni za ____ 1____ kiti cha ugavana katika kaunti ya Malabo zimekuwa na____ 2____ mkali mno. Wagombezi ____3____ wanazunguka eneo zima____ 4____ wapiga kura ili wawachague kuwa viognozi wao. ____5____ debe huku wakitoa ahadi za kuwasaidia____ 6____ kwa hali na mali. Kinachoshangaza ni kuwa hata gavana wa sasa anapiga kampeni licha ya kutotimiza ahadi alizotoa hapo ahali. Baada ya uchaguzi, mchaguliwa ____ 7____ kisha achukue hatamu____ 8____ uongozi. Ataanza ____ 9____ majukumu yake kama kiongozi baada ya kuapishwa.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. kubobea | B. kupigania | C. kuwania | D. kugombania |
| 2. | A. upinzani | B. wapinzani | C. mapinzani | D. pizani |
| 3. | A. wasaba | B. saba | C. nane | D. watisa |
| 4. | A. kueleza | B. kutaka | C. kuskukuma | D. kurai |
| 5. | A. Anajipigia | B. Walijipigia | C. Wanajipigia | D. Watajipigia |
| 6. | A. wakazi | B. watoro | C. wazalendo | D. walowezi |
| 7. | A. hula ahadi | B. hula kiapo | C. hula kalenda | D. huenda nguu |
| 8. | A. la | B. mwa | C. cha | D. za |
| 9. | A. kukeketa | B. kutekeleza | C. kutekeleza | D. kuteleza |

Sipendi jinsi____ 10____ tofauti ____ 11____ kikabila zimekuwa____ 12____ miongoni mwetu. Ikumbukwe kuwa ____ 13____. Iwapo tunatangamana katika shughuli zetu zote, mbona basi ____ 14____ kansa hii?____ 15____ hayo, tujue hatutaendelea kamwe tukibaguana. Kabila na rangi ni za utambuzi si ubaguzi.

10. A. ambapo B. ambayo C. ambako D. ambavyo
11. A. ya B. za C. cha D. wa
12. A. zikijikita B. zikijishaua C. zikijieleza D. zikinawiri
13. A. undugu ni kufaana si kufanana B. damu ni nzito kuliko maji C. mtaka cha mvunguni sharti ainame D. damu ni damu
14. A. tunaendelesha B. tuliendeleza C. tunaendeleza D. tutaendeleza
15. A. Kutokana na B. Fauka ya C. Bali ya D. Licha ya


**Kutoka swali la 16 hadi 30, chagua jibu sahihi**

16. **Andika wingi wa sentensi ifuatayo**

    Koo mwenye manyoya haba atauzwa.

    A. Koo wenye manyoya haba watauzwa.
    B. Makoo wenye manyoya haba watauzwa.
    C. Koo zenye manyoya mahaba watauzwa.
    D. Makoo wenye nyoya haba watauzwa.

17. Hili ni umbo gani?



    A. Tao B. Hiram
    C. Hilali D. Kipenyo

18. Chagua maneno ambayo yote ni vimilikishi

    A. hao, huyo, yule, kile
    B. haraka, ovyo, pole, mwakani
    C. ndimi, ndisi, ndio, ndiye
    D. yetu, langu, chake, vyenu

19. **Kinyume cha sentensi hii ni;**

    Mtwana anampelekea shaibu jimbi.

    A. Mjakazi anamrudishia ajuza koo.
    B. Mtwana hampelekei shaibu koo.
    C. Mjakazi anamrudishia ajuza jimbi.
    D. Mjakazi anampelekea ajuza jimbi.

20. **Jaza pengo kwa usahihi**

    Tumenunuliwa vijiko vipya vya________

    A. kula B. kuliwa
    C. kulia D. kukulia

21. "Kumvisha mtu kilemba cha ukoke" ni ________

    A. kumpiga mtu jeki
    B. kumdanganya mtu
    C. kumpa mtu sifa asizostahili
    D. kumpatia mtu pongezi

unaamuliwa na wewe mwenyewe na kwa haraka.

31. Kulingana na aya ya kwanza,ni jambo lipi ambalo limezua mdahalo mkubwa duniani?
    A. Umuhimu wa kujiajiri na mashaka ya kuajiriwa
    B. Mbinu mbadala za kujikimu maishani
    C. Swala la kuajiriwa au kujiajiri
    D. Watu wa umri mdogo kutafuta kazi za kuajiriwa
32. Mwandishi anaanza kwa kukiri kuwa
    A. kuajiriwi kuna faida nyingi kuliko kuajiriwa
    B. kujiajiri kunahitaji pesa nyingi ili kuanzisha biashara
    C. Kuajiriwa kuna manufaa kidogo kuliko kuajiriwa
    D. Kazi za kujiajiri zinataka taaluma na masomo mengi
33. Malipo unayopewa kwa kufanyia mtu kazi baada ya mwezi ni ________
    A. mtaji B. kiinuamgongo
    C. shokoa D. mshahara
34. Zifuatazo ni faida anazopata mtu ambaye amejiajiri ila ____________
    A. ana nafasi ya kujipatia utajiri na umaarufu
    B. huenda akatoa uamuzi mbaya ukaathiri biashara zake
    C. faida zote ni zake katika kampuni
    D. hasubiri hadi mwisho wa mwezi kulipwa
35. Usemi mwingine wenye maana sawa na "dhahiri shahiri" kwa mujibu wa habari hii ni ________
    A. liweliwalo B. ima fa ima
    C. kwa vyovyote vile D. waziwazi
36. Malengo na maono ya muda mrefu yanaweza kuwekwa na nani kulingana na mwandishi?
    A. Mtu aliyeajiri
    B. Mtu mwenye bishara nyingi
    C. Mtu aliyeajiriwa
    D. Mwenye maarifa na tajriba
37. Utamu wa kazi za kuajiriwa kulingana na taarifa hii ni ____________
    A. watu hushirikiana kufanya kazi kwa haraka
    B. adinasi kutoka pande mbalimbali za nchi hutangamana kazini
    C. aliyeajiriwa ana hakikisho la kupata mshahara mwisho wa mwezi
    D. waajiriwa huwa na uadilifu kazini
38. Ni nini kinaweza kusababisha ufujaji wa pesa katika kampuni ya aliyeajiri?
    A. Ikiwa hatakuwa na masomo ya chuo kikuu
    B. Iwapo atakosa taaluma katika mambo ya kuendesha biashara na uhasibu
    C. Ikiwa atajiingiza katika anasa za hapa na pale
    D. Kama wafanyakazi wake watamwibia mali yake
39. Wafanyakazi walioajiriwa huwajibika na huwa na uadilifu wanapofanya kazi. Hii ni kwa sababu
    A. wanaogopa kuachishwa kazi
    B. wana tajiriba ya kutosha kutekeleza kazi zao
    C. wanatafuta sifa na kupendwa na waajiri wao
    D. wanapenda kazi zao kwa dhati
40. Ni sababu gani hasa inayofanya mwandishi apendelee kuwa kazi za kujiajiri ni bora kuliko za kuajiriwa?
    A. Kazi za kujiajiri zina pato nono kuliko za kuajiriwa
    B. Watu katika kazi za kuajiriwa kupigwa kalamu mara kwa mara
    C. Aliyejiajiri huendesha biashara zake anavyotaka hata kama hatapata faida vizuri
    D. Kazi za kujiajiri zinampa mtu nafasi kubwa ya kujiamulia mambo na kupanga mikakati yake mwenyewe bila kushurutishwa na yeyote.

---

**Osman Dembele,**
**S.L.P 7034,**
**POPOTE.**
**5 - 5 - 2022**

**Kwa mpenzi Chikweze,**

Pokea salamu furifuri nikitumai kuwa u buheri wa afya na salama salimini huko mjini Cadiz. Zimepita siku ayami tangu nilipowatembelea huko, takribani mwongo mmoja. Yakini sijui nikufahamishe vipi kuhusu afya yangu. Somo tukikutana unione hutanitambua. Si barobaro yule uliyemjua mwenye urefu wa twiga na umbo la miraba minne. Leo hii ninakongoja. Nimekonda na kunyauka kiasi cha kwamba hata nauonea wivu unene wa sindano. Kwa hakika maisha ni mshumaa, unapozidi kuangaza ndivyo unavyozidi kuyeyuka na kumalizika.

Dunia ni mashaka makuu. Nina uchungu rohoni ninapokufahamisha kuwa nilichezea tope, nalo bila kusita lilinirukia. Niliteleza na nikaanguka nisiweze kusimama tena. Nifikiriapo kukueleza, kisunzi humzingira kiasi cha kuona maruerue.

Nilidhoofika kiafya kiasi cha kutotekeleza majukumu yangu kazini na bila shaka nikapigwa kalamu sasa miezi kenda imepita. Waliokuwa wandani waliingia mitini nisiwaone. Walinitenga na hata sasa wananipiga vijembe. Walisahau kuwa muazima yote ni Jalali Jalia ambaye ametujali kwa kuwa hali wali na akila hali wali mkavu.

22. Ukizidisha elfu moja mara elfu moja utapata
   A. laki moja B. elfu mia
   C. milioni moja D. milioni kumi


23. Sentesi "Asingekuja asingekupata" inamaanisha?
   A. alikuja na akakupata
   B. hakuja wala kukupata
   C. alikuja lakini hakukupata
   D. hakuja na kukupata

24. Methali gani kati ya hizi ambayo inahimiza uvumilivu?
   A. Mkono mmoja hauchinji ng'ombe.
   B. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.
   C. Kuchumbia si kuoa.
   D. Zito hufuatwa na jepesi.

25. Kutokana na kitenzi tulia tunapata sifa
   A. tulivu B. utulivi
   C. tuliza D. tulia

26. Ni ipi si maana ya neno **panda.**
   A. Makutano ya njia.
   B. Mdudu ajengaye utando.
   C. Paji la uso.
   D. Tia mbegu ardhini.

27. Taja vifaa vifuatavyo anavyotumia seremala.



   A. randa, sururu B. tupa, koleo
   C. msumeno, nyundo D. bisibisi, nyundo

28. Kimelea kinachosababisha uele wa malale ni ____
   A. kunguni B. mbu
   C. mbung'o D. ndorobo

29. Ni sentensi ili ambayo si sahihi?
   A. Huruma unaoponyesha ni mkuu
   B. Ndizi lililoiva ni lako.
   C. Mbuzi iliyokua nazi ni nzuri
   D. Pazia lililotundikwa limeoshwa

30. Neno lipi ambalo si nominoamata?
   A. Kombamwiko B. Askari jela
   C. Mwanasesere D. Rasilimali

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.**

Kuna njia nyingi za kujiendeleza na kujinufaisha kiuchumi. Walio katika umri wa kujitafutia pato la kila siku, afua ni mbili. Ujiajiri ama uajiriwe. Haya mambo mawili tangu jadi yamezua mdahalo mkubwa duniani. Swali na je, kati ya kuajiriwa na kujiariri, ni lipi bora?

Kujiajiri kuna manufaa makubwa zaidi kuliko kuajiriwa. Hakuna furaha inayozidi ile ya mtu anayetumia maarifa, ujuzi na tajriba yake na kuasisi kazi au biashara yake mwenyewe. Wewe ndiwe bosi wako mwenyewe. Huna wa kukupa masharti jinsi ya kuifanya kazi yako. Una uwezo wa kujipangia mambo yako mwenyewe mradi tu kazi yako izidi kunawiri. Uamuzi wote huwa ni wako. Kwa hivyo, utajitahidi kuhakikisha umeafikia malengo yako. Biashara inaponawiri, faida zote huwa zako. Kwa ufupi, ni wewe unayeendesha mambo na hakuna wa kukukanya ukitaka kupanua biashara zaidi.

Zaidi ya hayo, huna haja ya kusubiri mwezi uishe ndipo ulipwe mshahara kama ilivyo katika kazi za kuajiriwa. Hela zipo na ni wewe wa kupanga jinsi ya kuzitumia. Huhitaji kunyanyaswa au kijiingiza katika zile vuta nikuvute za mwajiri wa mwajiriwa wake. Aidha,kazi ya kujiajiri aghalabu hukupa nafasi au mwanya wa kujipatia utajiri mkubwa ambao unaweza kuandamana na umaarufu katika eneo fulani. Utajiri huo unaweza kutumiwa kuwasaidia watu wengine kupitia kwa ajira na huduma nyingine muhimu.

Kando na hayo, ni <u>dhahiri shahiri</u> kama pengo kuwa kujiajiri kuna manufaa mengi zaidi kuliko kuajiriwa. Pia kazi za kujiajiri zinampa adinasi ari ya kujipima uwezo wake wa kusimamia biashara au kutunza mali. Mja huyo pia anaweza kujiangalia na kujifunza kutokana na upungufu wake ikiwa utakuwapo.

Hata hivyo, kazi za kuajiriwa zina utamu wake. Mja aliyeajiriwa, ana hakikisho tosha la kupata mshahara <u>ima daima</u>. Hii ni kinyume na mtu aliyejiajiri ambaye wakati mwingine mambo <u>yakienda mrama</u> huenda akakosa hela anapozihitaji. Isitoshe, katika kazi za kujiajiri, mwenye kazi asipokuwa na taaluma katika mambo ya kuendesha biashara na uhasibu, kuna hatari ya kufuja pesa za kampuni.

Katika kazi za kuajiriwa kuna hali ya uwajibikaji na uadilifu katika kufanya kazi kwani kuna hatari ya kupigwa kalamu usipofanya kazi vizuri. Jambo hili huongezea kampuni mapato. Pia mwajiriwa hupata tajriba na ujuzi wa kufungua kazi yake.

Mwisho, kazi za kuajiriwa zinachangia kuleta ushirikiano, ujima na hali ya kutangamana kwa wafanyakazi kwani kampuni moja inaweza kuwa na zaidi ya mfanyakazi mmoja. Jambo hili huleta ufanisi na maendeleo.

Ni wazi kama mchana kwamba kazi za kujiajiri zina ubora zaidi ukilinganisha na kazi za kuajiriwa. Hii ni kwa sababu kazi za kujiajiri zinakupa nafasi kubwa ya kujiamulia mambo na kupanga mikakati yako mwenyewe bila kushurutishwa au kuangaliwa na yeyote. Aidha, uamuzi wa maswala nyeti kuhusu biashara

Mambo yaliniendea mrama. Kulipa kodi kukawa kugumu. Niliamua kuhamia mtaa wa mabanda, Nadama. Hali ya maisha hapa Nadama ni ngumu. Mazingira ni machafu, maadili yamezoroteka. Ninapowaona vijana mtaa huu wakirukia tope hukasirika sana.

Waraka huu nimeuandika kwa nia ya kukuomba msamaha. Niliasi maagano tuliyokuwa nayo pamoja ya kuheshimu ndoa yetu na kuanza tabia za nipe nikupe. Nilikuwa na jicho la nje lililofanya uchukie ndoa na kuamua kutoroka. Nilikuja hapa mjini kuchuma mali na badala yake nikachuma virusi. Kwa kweli, nilisafiria mtumbwi wa mfinyanzi.

Ninapofikiria kuwa wanangu wataitwa mayatima, huomba ardhi ipasuke niingie mzima mzima. Wasalamie hao wanangu Mesi na Ausu. Waeleze kuwa bado naikumbuka ahadi yangu ya kuwanunulia baiskeli. Iwapo nimedidimia katika lindi la ukata, ni lazima nitimize ahadi yangu.

Usiwaeleze hali ya uele wangu kwani ni ule usio na tiba. Watunze wana hao na mara kwa mara wazungumzie kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili.

---

41. Ni uhusiano upi ulioko kati ya mwandishi na mwandikiwa?
A. Ni mahasidi
B. Wanatoka katika ukoo mmoja
C. Ni wanandoa
D. Ni umbu

42. "Zimepita siku takribani mwongo mmoja kabla hatujaonana." Hii inamaanisha mwandishi amekaa muda gani kabla hajaonana na familia yake?
A. Karibu miaka ishirini
B. Kama miaka kumi hivi
C. Miaka kumi na miwili
D. Karibu miaka mitano

43. Mwandishi amekonda na kunyauka. Unafikiri ni nini sababu kuu ya hali hii yake?
A. Hana pesa za kununua chakula baada ya kupigwa kalamu
B. Alihamia mtaa wa mabanda ulio na mazingira machafu
C. Aliwaza sana kuhusu familia yake
D. Alikuwa na siha mbovu

44. Ni kauli ipi iliyo sahihi kulingana na habari hii?
A. Osman alihamia mtaa wa mabanda kwa sababu ya magonjwa
B. Osman alitimiza ahadi aliyowapa watoto wake kabla hajafa
C. Osman alitumia mtumbwi wa mtinyanzi kusafiri kutoka kijijini hadi mjini
D. Osman alikuwa na jicho la nje lililomsababishia hali mbaya anayopitia

45. Ni methali ipi kati ya hizi inayoweza kutumiwa kuelezea habari hii?
A. Fuata nyuki ukafe mzingani
B. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu
C. Chururu si ndondondo
D. Asiye na mwana aeleke jiwe

46. Kwa mujibu wa taarifa hii, ni dhahiri kuwa;
A. tabia za Chikweze zilimsababishia mwandishi anayoyapitia
B. hulka za mwandishi zilimueka katika hali duni ya maisha
C. Chikweze alimsamehe bwanake na kisha kurudiana
D. mwandishi alipiga dunia teke muda mfupi baada ya kuandika waraka

47. Dembele amesema kuwa wandani wake sasa wanampiga vijembe. Ni nini maana ya "kupiga vijembe?"
A. Wanamdharau
B. Wanatumia jembe kumpiga
C. Wanamsema kwa mafumbo
D. Wanamchukia

48. Maisha yamelinganishwa na mshumaa kwa kuwa;
A. maisha huishá kama mshumaa uishavyo unapozidi kuangaza
B. maisha huisha kama mshumaa uishavyo unapozidi kuangaza
C. maisha ya binadamu huyeyuka haraka kama mshumaa
D. mshumaa una maisha marefu kama ya binadamu

49. Kiini hasa cha Osman kuandika barua ni
A. kumsalimia mkewe na watoto
B. kujulia ninaye hali
C. kutakia familia yake baraka
D. kumwomba mkewe radhi

50. Mwandishi anamweleza mkewe asisitize kuhusu maadili anapozungumza na wanawe kwa nini?
A. Kuwa na maadili kulimfanya akafaulu maishani
B. Ni lazima mtu aliye na madili aishi maisha bora duniani
C. Kutokuwa na maadili humfanya mtu kupoteza familia yake
D. Kutozingatia maadili ndiko chanzo cha masaibu anayopitia